

Maendeleo ya Awali ya Mtoto

Zungumza na mtoto wako

Watoto wachanga hujifunza kuzungumza pale walezi wao wanapozungumza nao. Kuzungumza na mtoto wako mchanga ni muhimu kwa sababu

Kukusikiliza na kuzungumza nawe husaidia kukuza ubongo wa watoto wachanga.



Mtoto anayeweza kuwasiliana nawe hawi na msongo wa mawazo na huwa na uwezekano mdogo wa kulia.



Kumsikiliza na kuzungumza na mtoto wako mchanga husaidia kujenga uhusiano wa karibu pamoja naye.



Mtoto kuweza kuzungumza mapema humsaidia kuja kufanya vizuri shuleni na kufaulu maishani hapo baadaye.



Idadi ya maneno ambayo watoto wachanga husikia huchangia sana katika uwezo wao wa kuzungumza mapema. Utafiti unaonyesha kuwa nchini Tanzania watu hutumia maneno 63 tu kwa saa wakati wa kuzungumza na watoto wao wachanga. Hii inalinganishwa na maneno 600-800 kwa saa yanayotumika Uingereza na USA. Jaribu kuzungumza na mtoto wako mara nyingi zaidi wakati wa :



Kuwalisha



Kabla ya kulala



Kucheza nao



Kuwabadilisha nepi



Kuwafundisha tabia njema



Wakati mtoto anapojaribu kutoa sauti